# TAARIFA KWA UMMA

## Hilda Bujiku ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Fedha, Vodacom Tanzania Plc

**November 19, 2021, Dar es salaam**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Vodacom Tanzania Plc, Jaji (Mstaafu) Thomas B. Mihayo anayofuraha kutangaza uteuzi wa Hilda Bujiku kuwa Mkurugenzi mpya wa Fedha kuanzia Januari 1, 2022.

Hilda kwa sasa ni Naibu Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania PLC toka Aprili 2021. Hapo awali alikuwa Mtendaji Mkuu anayehusika na Mipango na Uchambuzi wa Fedha, Mahusiano ya Wawekezaji na Sekretarieti ya Kampuni.

SOLOMON Stockbrokers

Alijiunga na Vodacom Tanzania mwaka 2012 na kushika nyadhifa mbalimbali za juu katika kampuni hiyo. Alifanya kazi kama Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania kwa muda wa miezi 8 mwaka 2014 na baadaye kuhamia Vodacom Lesotho kama Mkurugenzi wa Fedha. Akiwa Lesotho, alitekeleza kwa ufanisi miradi ya mabadiliko na kuonyesha thamani thabiti kwa wanahisa.

Bodi inachukua fursa hii kumshukuru Jacques Marais kwa kujitoa kwake na mchango wake muhimu kwa biashara na yote aliyofanikisha kwa miaka 5 kama Mkurugenzi wa Fedha na kumtakia kila la heri katika majukumu yake ya baadaye.



**Pamoja tunaweza**

vodacom